MIDTERM

G6

MTAALA WA UMILISI

Muda: Saa 1 dakika 40

SEHEMU YA KWANZA:
KISWAHILI - LUGHA

Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 1-5.



Tuta na Twita walikuwa wavulana. Walipendana kama chanda na pete. Walisoma katika shule moja. Ajabu ni kwamba wote walikuwa na umri sawa. Walikuwa wakisoma kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Jumamosi na Jumapili walipumzika nyumbani kwao na kufanya kazi za ziada kutoka shuleni. Baada ya kumaliza kazi za ziada, walipendelea kuenda kucheza.

Siku moja Tuta na Twita waliamua kwenda msituni kuwinda ndege kwa manati. Ilikuwa siku ya Jumapilii. Walipofika msituni,waliendelea kuwawinda ndege. Waliendelea na mchezo wao hadi masaa ya adhuhuri. Tuta akamwuliza Twita," Rafiki yangu,tutakula nini? Mimi ninahisi njaa!" Twita akasema "Mimi nina kiporo ndani ya mfuko wa kaptura yangu. Sina wasiwasi!"

Maswali

1. Tuta na Twita walikuwa wavulana ndiko kusema

   A. walikuwa vijana

   B. walikuwa watoto wa kiume

   C. walikuwa duma

   D. walikuwa wanaume.

2. Walipendana kama chanda na pete inamaanisha

   A. walipendana sana

   B. walipendana kidogo tu

   C. walipenda pete na chanda

   D. walikuwa wapenzi.